

Hali ya Hatari-Mozambique

TAARIFA iliyotolewa na chama cha Frelimo iliyo-tiwa sahihi na Bwana Paul J. Bayeke, Makamu katibu wa utoaji habari kwenye ofisi hiyo inasema kuwa hali iliyopo sasa huko Mozambique ni hali ya hatari kabisa. *Nguzummo 30th July, 63*

Taarifa hiyo ikaongeza kuwa, Mreno siku hizi anafanya vitendo ambavyo sio hata halali kute ndewa mwanadamu yoyote, kwani wananchi wa huko wanapigwa ovyo bila ya kosa lolote, viongozi wengi wa Frelimo katika nchi hiyo wamechukuliwa na kupakiwa katika ndege na haijulikani wanapelekwa wapi pia jamaa ambao walifungwa kwa ajili ya siasa nao kadhalika wamechukuliwa na haijulikani wamepelekwa wapi.

Apigwa risasi

Katika kijiji kimoja kiiitwacho Niula mama mmoja alipigwa risasi wakati majesji ya Kireno yalipokuwa wakifanya majaribio ya ma-

bom na silaha kwa kupiga mizinga. Bwana mmoja naye kadhalika alikamatwa na Serkali ya Kireno na kupigwa na mpini wa bunduki na akafariki dunia hapo hapo.

Kuna kimbunga pia cha kuwakamata jamaa wote watokao Tanga nyika, na kuweza kuu lizwa maswali mengi huku wakipigwa na kuadhibiwa vikali mpa ka wengine kupata majeraha makaii, ikamaliza taarifa hiyo kuwa, hayo yote yanatokana kwa ajili ya kadi za Frelimo ambazo zimepelekwa huko hivi karibuni, kwani wananchi wanakatazwa kujitetea.